Haqiyqat-ut-Tawhiyd wash-Shirk

[Uhakika wa Tawhiyd na Shirki]

Mwandishi:

Imaam ´Abdul-´Aziyz bin ´Abdillaah bin Baaz

Tarjama:

Abu Bakr Khatwiyb al-Atrush

01. Lengo la kuumbwa majini na watu....3
02. Baadhi ya sifa za Allaah (Subhanaahu wa Ta´ala)....9
03. Ni lazima kumuamini Allaah na kuwasadikisha Mitume Wake....13
04. Ulazima wa kuwaamini Mitume wote....16
05. Maana ya Uislamu....17
06. Ndio maana mayahudi na manaswara wakakufuru....18
07. Kinyume cha Tawhiyd ni shirki....19
08. Maana ya Shahaadah....20
09. Kuhukumu kwa Shari´ah ni sehemu katika Tawhiyd....22
10. Baadhi ya sura za shirki na kufuru....23
11. Maana ya ´ibaadah....25
12. Uwajibu wa kuwasadikisha Mitume wote na ukafiri wa anayedai utume na wafuasi wake....26
13. Kitenguzi kimoja cha Uislamu kinabatilisha matendo yote....27
14. Watu walivyoipuuza elimu ya dini hii leo....29
15. Hukumu ya mwenye kufa katika shirki kubwa na madhambi....30
16. Muislamu kutenga wakati kwa ajili ya kujifunza dini yake....32
17. Shirki ndogo na aina zake....34

01. Lengo la kuumbwa majini na watu

Himdi zote anastahiki Allaah, Mola wa walimwengu. Hapana uadui isipokuwa kwa madhalimu. Swalah na salaam zimwendee mja na Mtume wake ambaye ndiye kiumbe Chake bora kabisa na mwaminifu juu ya Wahy. Naye si mwengine ni kiongozi wetu, bwana wetu Muhammad bin ´Abdillaah bin ´Abdil-Muttwalib kutoka katika ukoo wa Haashim Makkah halafu akahamia al-Madiynah, kizazi chake, Maswahabah wake na wale watakaofuata njia yake na uongofu wake mpaka siku ya Qiyaamah.

Amma ba´d:

Allaah (´Azza wa Jall) amewaumba viumbe ili wamuabudu Yeye pekee na amewatuma Mitume ili wabainishe hekima hii na kulingania kwayo, wabainishe upambanuzi wake na wabainishe vilevile yale yanayopingana nayo. Namna hii ndivyo vilivyokuwa vitabu vya kimbingu na wakatumwa Mitume wa kibinaadamu kutoka kwa Allaah (´Azza wa Jall) kuwaendea majini na watu. Allaah (Subhaanah) amefanya dunia hii kuwa ni njia ya kuiendea Aakhirah na yenye kuiabiria. Atakayeimarisha kwa kumtii Allaah kwa kumpwekesha na kumfuata Mtume Wake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), basi atatoka katika nyumba ya matendo– ambayo ni dunia – na kwenda katika nyumba ya malipo – ambayo ni Aakhirah – na atakuwa katika nyumba ya neema, furaha, heshima na raha. Ni nyumba zisizoisha neema zake, watu wake hawafi, nguo zao haziishi na wala ujana wao hauumbwi. Bali watakuwa katika neema daima, afya njema daima, ujana wenye kudumu, maisha mazuri na yenye furaha ambapo neema zake haziishi. Allaah (´Azza wa Jall) atawanadia:

“Enyi watu wa Peponi! Hakika nyinyi mtaendelea kuwa hai na hamtokufa kamwe, mtakuwa na afya njema na hamtopatwa na ugonjwa kamwe,

mtaendelea kushiba na wala hamtopatwa na njaa kamwe na mtaendelea kuneemeshwa na wala hamtokatishwa tamaa kamwe."[1]

Hii ndio hali yao. Humo watapata wanayotamani na wanayoomba:

نُزُلًا مِّنْ غَفُورٍ رَّحِيمٍ

"Ni takrima kutoka kwa mwingi wa kusamehe, Mwenye huruma." (31:32)

Humo watakutana na Allaah (´Azza wa Jall) vile anavyotaka na wataona Uso Wake mtukufu (Jalla wa ´Alaa).

Kuhusu wale wenye kwenda kinyume na Mitume hapa duniani kwa kufuata matamanio ya shaytwaan, watatoka katika dunia hii na wende katika nyumba ya malipo, nyumba ya udhalilishaji na khasara, adhabu, maumivu na Moto ambayo watu wake watakuwa katika adhabu na khasara yenye kudumu:

لَا يُقْضَىٰ عَلَيْهِمْ فَيَمُوتُوا وَلَا يُخَفَّفُ عَنْهُم مِّنْ عَذَابِهَا

"Hawatahukumiwa kifo ili wafe na wala hawatakhafifishiwa adhabu yake." (35:36)

إِنَّهُ مَن يَأْتِ رَبَّهُ مُجْرِمًا فَإِنَّ لَهُ جَهَنَّمَ لَا يَمُوتُ فِيهَا وَلَا يَحْيَىٰ

"Hakika yule atayemjia Mola wake akiwa mhalifu, basi atapata Moto wa *Jahannam* - hatokufa humo na wala hatoishi." (20:74)

وَإِن يَسْتَغِيثُوا يُغَاثُوا بِمَاءٍ كَالْمُهْلِ يَشْوِي الْوُجُوهَ ۚ بِئْسَ الشَّرَابُ وَسَاءَتْ مُرْتَفَقًا

"Wakiomba uokozi watasaidiwa kwa kupewa maji kama mafuta yaliyotibuka yanayobabua nyuso - Ubaya ulioje kinywaji hicho na uovu ulioje mahali pa kupumzikia!" (18:29)

وَسُقُوا مَاءً حَمِيمًا فَقَطَّعَ أَمْعَاءَهُمْ

"Wakinyweshwa maji yachemkayo yakikatakata machango yao." (47:15)

[1] Muslim (2837), at-Tirmidhiy (3246), Ahmad (03/95) na ad-Daarimiy (2821).

Makusudio ni kwamba nyumba hii ni ya malipo, nyumba ya kujikurubisha kwa Allaah (´Azza wa Jall) kwa yale yanayomridhisha, nyumba ya kupambana na nafsi, nyumba ya kuhesabiwa, nyumba ya kujifunza na kuielewa dini, nyumba ya kusaidiana katika wema na uchaji, nyumba ya kuusiana kwa haki na kusubiri, elimu na matendo na kupambana Jihaad. Allaah (Subhaanahu wa Ta´ala) amesema:

وَمَا خَلَقْتُ الْجِنَّ وَالْإِنسَ إِلَّا لِيَعْبُدُونِ مَا أُرِيدُ مِنْهُم مِّن رِّزْقٍ وَمَا أُرِيدُ أَن يُطْعِمُونِ إِنَّ اللَّهَ هُوَ الرَّزَّاقُ ذُو الْقُوَّةِ الْمَتِينُ

“Sikuumba majini na watu isipokuwa waniabudu. Sitaki kutoka kwao riziki yoyote na wala sitaki wanilishe. Hakika Allaah ndiye Mwingi wa kuruzuku, Mwenye nguvu madhubuti.” (51:56-58)

Allaah amewaumba watu na majini ili wamuabudu (´Azza wa Jall). Hakuwaumba (Subhaanah) kwa kuwa anawahitajia. Hakika Yeye (Subhaanah) ni mkwasi kwa dhati Yake kutokamana na kila kisichokuwa Yeye. Amesema (Subhaanah):

يَا أَيُّهَا النَّاسُ أَنتُمُ الْفُقَرَاءُ إِلَى اللَّهِ ۖ وَاللَّهُ هُوَ الْغَنِيُّ الْحَمِيدُ إِن يَشَأْ يُذْهِبْكُمْ وَيَأْتِ بِخَلْقٍ جَدِيدٍ وَمَا ذَٰلِكَ عَلَى اللَّهِ بِعَزِيزٍ

“Enyi watu! Nyinyi ni mafakiri kwa Allaah na Allaah ndiye Mkwasi, anayestahiki kuhimidiwa. Akitaka atakuondosheni mbali na kuleta viumbe vipya - na hayo kwa Allaah si makubwa.” (35:15-17)

Hakuwaumba ili awe na ukuu kutokamana na udogo au atukuke kutokamana na udhalilifu. Lakini hata hivyo amewaumba (Subhaanahu wa Ta´ala) kwa hekima kubwa; wamuabudu, wamuadhimishe, wamche, wamsifu (Subhaanahu wa Ta´ala) kwa yale anayostahiki, wajifunze majina na sifa Zake na wamsifu kwavyo, wamwelekee kwa yale maneno na vitendo vilivyo vya wajibu, wamshukuru kwa neema Zake, wasubiri kwa yale anayowajaribu, wapambane katika njia Yake, wazingatie ukubwa Wake na yale matendo yanayowastahiki. Amesema (´Azza wa Jall):

اللَّهُ الَّذِي خَلَقَ سَبْعَ سَمَاوَاتٍ وَمِنَ الْأَرْضِ مِثْلَهُنَّ يَتَنَزَّلُ الْأَمْرُ بَيْنَهُنَّ لِتَعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ وَأَنَّ اللَّهَ قَدْ أَحَاطَ بِكُلِّ شَيْءٍ عِلْمًا

“Allaah ndiye kaumba mbingu saba na katika ardhi mfano wake, inateremka amri baina yavyo ili mjue kuwa Allaah juu ya kila jambo

ni Muweza na kwamba Allaah amekwishakizunguka kila kitu kwa ujuzi." (65:12)

وَلِلَّهِ الْأَسْمَاءُ الْحُسْنَىٰ فَادْعُوهُ بِهَا

"Allaah ana majina mazuri kabisa, hivyo basi muombeni kwayo." (07:180)

إِنَّ فِي خَلْقِ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ وَاخْتِلَافِ اللَّيْلِ وَالنَّهَارِ لَآيَاتٍ لِّأُولِي الْأَلْبَابِ الَّذِينَ يَذْكُرُونَ اللَّهَ قِيَامًا وَقُعُودًا وَعَلَىٰ جُنُوبِهِمْ وَيَتَفَكَّرُونَ فِي خَلْقِ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ رَبَّنَا مَا خَلَقْتَ هَٰذَا بَاطِلًا سُبْحَانَكَ فَقِنَا عَذَابَ النَّارِ

"Hakika katika kuumbwa mbingu na ardhi na kubadilika kwa usiku na mchana, bila shaka ni alama kwa wenye akili; ambao wanamdhukuru Allaah kwa kusimama, na kwa kukaa na kwa kulala ubavuni mwao na wanazingatia katika kuumbwa mbingu na ardhi [na huku wakisema]: "Mola wetu, hukuumba haya bure. Utakasifu ni Wako! Tukinge na adhabu ya moto."" (03:190-191)

Mja wa Allaah! Hakika wewe umeumbwa katika dunia hii sio kwa lengo la kubaki na kudumu ndani yake. Umeumbwa ili uweze kuhamishwa kutoka ndani yake baada ya matendo. Huenda ukahamishwa kutoka ndani yake kabla ya matendo ilihali bado mtoto hujabaleghe na hujawajibikiwa na matendo kutokana na hekima kubwa. Tunachotaka kusema ni kwamba dunia ni nyumba iliyochanganyika na shari na kheri, wema na wasiokuwa wema, makadirio, furaha, mambo yenye manufaa na yenye madhara. Ndani yake mna mzuri na mbaya, mgonjwa na mwenye afya njema, tajiri na fakiri, kafiri na muumini, mtenda dhambi na aliyenyooka na vilevile ndani yake mna viumbe mbalimbali vilivyoumbwa kwa ajili ya manufaa kwa majini na wanaadamu. Amesema (Ta´ala):

هُوَ الَّذِي خَلَقَ لَكُم مَّا فِي الْأَرْضِ جَمِيعًا

"Yeye ndiye kakuumbieni vyote vilivyomo ardhini." (02:29)

Makusudio ya viumbe hivi ni kama tulivyotangulia kusema wamuadhimishe Allaah, wamtii katika dunia hii, waadhimishe maamrisho Yake na makatazo Yake, wamuabudu pekee (Subhaanahu wa Ta´ala) kwa kutii maamrisho Yake na kujiepusha na makatazo Yake na wamlenge Yeye (Subhaanah) katika

kutafuta mahitaji mbalimbali, wakati wa majanga na malalamiko yote apelekewe Yeye, kuomba uokozi kutoka Kwake na msaada pia katika kila kitu na vilevile katika kila jambo la kidunia na Aakhirah.

Mja wa Allaah! Kinachokusudiwa ni kwamba lengo la wewe kuumbwa kwako ni kumpwekesha (Subhaanah), kuadhimisha maamrisho na makatazo Yake na umkusudie Yeye peke katika mahitaji Yako, kumtaka msaada katika mambo ya dini na dunia yako na ufuate yale waliyokuja nayo Mitume Wake na ujisalimishe nayo hali ya kutii na kwa kutaka mwenyewe, kupenda yale aliyokuamrisha, kuchukia yale aliyokukataza na wakati huo huo uwe ni mwenye kutaraji rehema za Mola Wako na unaogopa adhabu Yake (Subhaanahu wa Ta´ala).

Mitume wametumwa kwa viumbe ili wawajuze haki hii na wawafunze yale yaliyo ya wajibu juu yao na yale ya haramu juu yao ili wasije kusema kuwa hawakujiwa na mtoa bishara wala muonyaji yeyote. Uhakika wa mambo ni kwamba walijiwa na Mitume wenye kutoa bishara njema na wenye kuonya. Amesema (Subhaanah):

وَلَقَدْ بَعَثْنَا فِي كُلِّ أُمَّةٍ رَّسُولًا أَنِ اعْبُدُوا اللَّهَ وَاجْتَنِبُوا الطَّاغُوتَ

"Hakika tulituma katika kila ummah Mtume [awaamrishe watu wake] kwamba: "Mwabuduni Allaah na jiepusheni na twaaghuut [miungu ya uongo]."" (16:36)

رُّسُلًا مُّبَشِّرِينَ وَمُنذِرِينَ لِئَلَّا يَكُونَ لِلنَّاسِ عَلَى اللَّهِ حُجَّةٌ بَعْدَ الرُّسُلِ

“Mitume wenye kutoa bishara njema na waonyaji ili pasikuweko kutoka kwa watu hoja yoyote juu ya Allaah baada ya [kutumwa] Mitume.” (04:165)

وَمَا أَرْسَلْنَا مِن قَبْلِكَ مِن رَّسُولٍ إِلَّا نُوحِي إِلَيْهِ أَنَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا أَنَا فَاعْبُدُونِ

"Hatukutuma kabla yako Mtume yeyote isipokuwa Tulimfunulia Wahy ya kwamba: "Hakika hapana mungu wa haki isipokuwa Mimi - basi niabuduni!"" (21:25)

Wametumwa ili wawaelekeze majini na watu kwa yale waliyotumwa na wawaelekeze katika zile sababu za uokozi na wawaelekeze vilevile zile sababu za maangamivu na vilevile wawasimamishie hoja na wawakatie udhuru. Allaah (Subhaanahu wa Ta´ala) anapenda kusifiwa na kwa ajili hiyo ndio maana amejisifu Mwenyewe kwa yale anayostahiki. Vilevile ni Mwenye wivu juu ya yale aliyoharamisha na kwa ajili hiyo ndio maana ameharamisha machafu kuanzia yale yenye kuonekana na yaliyojificha.

Kwa ajili hiyo ni juu yako umtape (Subhaanah) na umsifu kwa yale anayostahiki. Himdi zote ni Zake duniani na Aakhirah. Ni juu yako kumsifu kwa majina na sifa Zake, umshukuru kwa neema Zake na usubiri kwa yale yenye kukusibu pamoja na kufanya sababu alizokuwekea Allaah na kukuhalalishia nazo. Ni juu yako kuyaheshimu yale Aliyokuharamishia na ujiepushe nayo, usimame katika mipaka Yake hali ya kumtii (Subhaanahu wa Ta´ala) na yale waliyokuja nayo Mitume (Swalla Allaahu ´alayhim wa sallam). Ni juu yako kuielewa dini yako, kujifunza yale uliyoumbwa kwa ajili yake na uwe na ustahamilivu juu ya hayo ili uweze kutekeleza mambo ya wajibu kwa elimu na ujuzi. Amesema (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

“Yule ambaye Allaah anamtakia kheri basi humpa ufahamu katika dini.”[2]

“Mwenye kuchukua njia akitafuta elimu ndani yake, basi Allaah humsahilishia njia ya kuelekea Peponi.”

Ameipokea Muslim katika “as-Swahiyh” yake.

[2] al-Bukhaariy (71), Muslim (1037), Ibn Maajah (221), Ahmad (04/93), Maalik katika “al-Muwattwaa´” (1667) na ad-Daarimiy (226).

02. Baadhi ya sifa za Allaah (Subhanaahu wa Ta´ala)

Amrisho kubwa na muhimu zaidi ni kumpwekesha (Subhaanah) na kuacha kumshirikisha (´Azza wa Jall). Hili ndio jambo muhimu zaidi na ndio msingi wa dini ya Uislamu. Ndio dini ya Mitume wote kuanzia wa mwanzo hadi wa mwisho wao; nayo ni kumpwekesha Allaah na kumtakasia ´ibaadah Yeye badala ya wengine wote. Huu ndio msingi wa dini na ndio dini ya Mitume wote kuanzia wa mwanzo wao, ambaye ni Nuuh, mpaka wa mwisho wao, ambaye ni Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Allaah hakubali dini kutoka kwa yeyote isipokuwa hii; ambayo ni Uislamu.

Umeitwa ´Uislamu` kwa kuwa ndani yake kuna kujisalimisha kwa Allaah, kumdhalilikia, kumuabudu na kumnyenyekea. Uislamu ni kumpwekesha na kumtakasia Yeye hali ya kumtakasia Yeye (Jalla wa ´Alaa). Umeusalimisha uso wako kwa Allaah, umemtakasia matendo yako Yeye na umeuelekeza uso wako kwa Allaah katika mambo yako ya siri na ya dhahiri, khofu na matarajio yako, maneno na vitendo vyako na katika kila kitu. Jifunze ya kwamba Yeye (Subhaanah) ndiye mungu wa haki anayestahiki kuabudiwa, kutiiwa na kuadhimishwa. Hapana mungu wa haki isipokuwa Yeye na wala hapana mola asiyekuwa Yeye. Kinachotofautiana ni zile Shari´ah. Amesema (Ta´ala):

لِكُلٍّ جَعَلْنَا مِنكُمْ شِرْعَةً وَمِنْهَاجًا

“Kwa kila [Ummah] katika nyinyi Tumeujaalia Shari´ah na mfumo wake.” (05:48)

Kuhusu dini ya Allaah ni moja; nayo ni Uislamu ambao maana yake ni kumtakasia ´ibaadah Allaah peke yake. Kumtakasia ´ibaadah inahusiana na du´aa, khofu, matarajio, kumtegemea, shauku, woga, swalah, swawm na mengineyo. Amesema (Subhanaahu wa Ta´ala):

وَقَضَىٰ رَبُّكَ أَلَّا تَعْبُدُوا إِلَّا إِيَّاهُ

"Mola wako ameamrisha, kwamba asiabudiwe yeyote isipokuwa Yeye pekee."" (17:23)

Bi maana ameamrisha asiabudiwe mwengine isipokuwa Yeye.

إِيَّاكَ نَعْبُدُ وَإِيَّاكَ نَسْتَعِينُ

“Wewe pekee ndiye tunakuabudu na Wewe pekee tunakuomba msaada." (01:05)

Amewaeleza waja Wake haya ili wayaseme na wayatambue. Amewafunza namna ya kumsifu. Amesema (´Azza wa Jall):

الْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ مَالِكِ يَوْمِ الدِّينِ

“Himdi zote anastahiki Allaah, Mola wa walimwengu. Mwingi wa rehema, Mwenye kurehemu, [ambaye ni] Mfalme wa siku ya malipo!” (01:02-04)

Amewafunza sifa hizi kubwa. Halafu akasema:

إِيَّاكَ نَعْبُدُ وَإِيَّاكَ نَسْتَعِينُ

“Wewe pekee ndiye tunakuabudu na Wewe pekee tunakuomba msaada." (01:05)

Haya yamuelekea Yeye (Subhaanahu wa Ta´ala) na kumsifu kwa yale anayostahiki na kutambua kuwa Yeye ndiye Mola wa walimwengu, Mwenye kuwatendea wema, Mwenye kuwalea kwa neema Zake, kwamba Yeye ndiye Mwingi wa huruma, Mwenye kurehemu na kwamba Yeye ndiye Mfalme wa siku ya malipo. Zote hizi ni haki za Mola wetu (´Azza wa Jall). Halafu akasema:

إِيَّاكَ نَعْبُدُ وَإِيَّاكَ نَسْتَعِينُ

“Wewe pekee ndiye tunakuabudu na Wewe pekee tunakuomba msaada." (01:05)

Wewe pekee ndiye tunakuabudu na Wewe pekee ndiye tunakutaka msaada. Hakuna Mola wala mtakwa msaada asiyekuwa Wewe. Yale yote yanayowatokea waja ni yenye kutoka kwa Allaah. Yeye ndiye kawasahilishia na Yeye ndiye kawaandalia, kuwasaidia nayo na akawapa nguvu kwa hayo. Kwa ajili hiyo anasema (Jalla wa ´Alaa):

وَمَا بِكُم مِّن نِّعْمَةٍ فَمِنَ اللَّهِ

“Neema yoyote mliyo nayo, basi ni kutoka kwa Allaah.” (16:53)

Yeye (Subhaanah) ndiye Mneemeshaji na Mwenye kutakwa msaada na vilevile Mwenye kuabudiwa kwa haki.

Mja! Ukipata neema, sawa iwe kubwa au ndogo, mtumwa na mfalme na vinginevyo vyote ni katika neema za Allaah (Jalla wa ´Alaa). Yeye ndiye karahisisha hivyo (Subhaanahu wa Ta´ala). Ameiumba Yeye kupitia mikono ya yule mwenye kukuletea nayo. Yeye ndiye ameufanya moyo wake kuweza kukuletea nayo. Yeye ndiye kampa nguvu, moyo na akili hizo. Allaah ndiye ameweka kwenye moyo wake kitu mpaka akaweza kukufikishia nayo. Neema zote ni zenye kutoka kwa Allaah pasi na kujali njia iliyotumika. Yeye ndiye muabudiwa wa haki. Yeye ndiye muumbaji wa viumbe. Yeye ndiye Mwenye kuwalea kwa neema Zake. Yeye ndiye Mwenye kuhukumu baina yao duniani na Aakhirah. Yeye ni Mwenye kusifiwa kwa sifa kamilifu na Mwenye kutakaswa kwa sifa zote pungufu na kasoro. Amepwekeka katika uola Wake. Amepwekeka katika uungu Wake. Amepwekeka katika majina na sifa Zake (Jalla wa ´Alaa). Yeye (Subhaanah) amepwekeka kwa njia zote na ana umoja katika kuwaumba viumbe, kuwaendesha, kuwaruzuku na kuyaendesha mambo yao. Hakuna yeyote anayeshirikiana Naye katika hayo (Subhaanahu wa Ta´ala). Amesema (´Azza wa Jall):

اللَّهُ خَالِقُ كُلِّ شَيْءٍ ۖ وَهُوَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ وَكِيلٌ

“Allaah ndiye Muumbaji wa kila kitu - Naye juu ya kila kitu ni mtegemewa.” (39:62)

إِنَّ اللَّهَ هُوَ الرَّزَّاقُ ذُو الْقُوَّةِ الْمَتِينُ

“Hakika Allaah ndiye Mwingi wa kuruzuku, Mwenye nguvu madhubuti.” (51:58)

إِنَّ رَبَّكُمُ اللَّهُ الَّذِي خَلَقَ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضَ فِي سِتَّةِ أَيَّامٍ ثُمَّ اسْتَوَىٰ عَلَى الْعَرْشِ ۖ يُدَبِّرُ الْأَمْرَ ۖ مَا مِن شَفِيعٍ إِلَّا مِن بَعْدِ إِذْنِهِ ۚ ذَٰلِكُمُ اللَّهُ رَبُّكُمْ فَاعْبُدُوهُ ۚ أَفَلَا تَذَكَّرُونَ إِلَيْهِ مَرْجِعُكُمْ جَمِيعًا

“Hakika Mola wenu ni Allaah ambaye ameumba mbingu na ardhi katika siku sita kisha akalingana juu ya ´Arshi. Anayaendesha mambo. Hakuna mwombezi yeyote isipokuwa baada ya idhini Yake. Huyu ndiye Allaah Mola Wenu, basi mwabuduni. Je, hamkumbuki? Kwake ndiko marejeo yenu nyote.” (10:03-04)

Yeye ndiye Mwenye kustahiki kuabudiwa kwa kukamilika kwa neema Zake, wema Wake na kwa kuwa Yeye ndiye Muumbaji, Mruzukaji na kwa sababu vilevile Yeye ndiye Mwenye kuwaendesha na kuwapeleka viumbe na kwa sababu pia Yeye ni mkamilifu katika dhati Yake, sifa na majina Yake. Kwa ajili hii ndio maana amestahiki ´ibaadah juu ya viumbe wote na wanastahiki kumnyenyekea. ´Ibaadah ni kule kunyenyekea na kudhalilika.

Dini imeitwa kuwa ni ´ibaadah kwa kuwa mja anaitekeleza kwa kumnyenyekea Allaah na kujidhalilisha mbele Yake. Ndio maana Uislamu ukaitwa kuwa ni ´ibaadah.

03. Ni lazima kumuamini Allaah na kuwasadikisha Mitume Wake

Mja ni yule mdhalili ambaye ananyenyekea kwa Allaah ambaye anayaadhimisha makatazo Yake. Kadri ambavyo mja atakuwa anamtambua Allaah kikamilifu zaid ndipo atamuamini kikamilifu zaidi na kumuabudu kikamilifu zaidi. Kwa ajili hii ndio maana Mitume (Swalla Allaahu ´alayhim wa sallam) walikuwa ni watu wenye ´ibaadah kamilifu zaidi. Kwa kuwa wao ndio wanaomtambua na kumjua Allaah zaidi. Vilevile ndio wenye kumuadhimisha zaidi kuliko wengine wote – swalah na salaam ziwe juu yao wote. Kwa ajili hii ndio maana Allaah amemsifu Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kwa uja katika nafasi tukufu zaidi. Amesema (Subhaanah):

سُبْحَانَ الَّذِي أَسْرَىٰ بِعَبْدِهِ

“Utakasifu ni wa Ambaye amemsafirisha usiku mja Wake.” (17:01)

الْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي أَنزَلَ عَلَىٰ عَبْدِهِ الْكِتَابَ

“Himdi zote anastahiki Allaah ambaye amemteremshia mja Wake Kitabu.” (18:01)

وَأَنَّهُ لَمَّا قَامَ عَبْدُ اللَّهِ يَدْعُوهُ كَادُوا يَكُونُونَ عَلَيْهِ لِبَدًا

”Na kwamba aliposimama mja wa Allaah kumwomba walikaribia kumzonga.” (72:19)

Kuna Aayah zingine mbali na hizi.

Uja ndio nafasi kubwa na tukufu zaidi. Halafu Allaah akawazidishia fadhila kutoka Kwake (Subhaanah) kwa ujumbe aliowatuma nao. Wakakusanya fadhila mbili:

Ya kwanza: Fadhila ya ujumbe.

Ya pili: Fadhila ya uja maalum.

Watu wakamilifu zaidi katika kumuabudu na kumwogopa Allaah ni Mitume na Manabii (Swalla Allaahu ´alayhim wa sallam).

Halafu wanafuata wakweli ambao umekamilika ukweli wao kwa Allaah na kwa Mitume wake, wakawa na msimamo juu ya maamrisho Yake na hivyo wakawa watu bora baada ya Mitume (Swalla Allaahu ´alayhim wa sallam). Anayeshika msitari wa mbele kabisa ni Abu Bakr as-Swiddiyq (Radhiya Allaahu ´anh). Yeye ndiye kiongozi wa wakweli na mkamilifu zaidi wa ukweli kwa sababu ya fadhila, kumcha kwake Allaah, kutangulia kwake mbele katika mambo ya kheri na kusimama na maamrisho ya Allaah ipasavyo. Vilevile kwa sababu yeye ndiye rafiki yake na Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), aliyesuhubiana naye pangoni na aliyemsaidia kiasi na uwezo na nguvu zake zote (Radhiya Allaahu ´anh).

Tunachotaka kusema ni kwamba nafasi ya uja na nafasi ya ujumbe ndio nafasi tukufu zaidi. Ubora wa utume ukiondoka kunabaki nafasi ya ukweli wa ´ibaadah. Watu walio na imani, wema, uchaji na uongofu zaidi ni Mitume (Swalla Allaahu ´alayhim wa sallam). Hili ni kwa sababu ya ujuzi wao mkamilifu wa kumtambua Allaah, kumuabudu kwao na kudhalilikia ukubwa Wake (Jalla wa ´Alaa).

Halafu wanafuata wakweli, kisha mashahidi kisha waja wema kwa jumla. Amesema (Jalla wa ´Alaa):

وَمَن يُطِعِ اللَّهَ وَالرَّسُولَ فَأُولَٰئِكَ مَعَ الَّذِينَ أَنْعَمَ اللَّهُ عَلَيْهِم مِّنَ النَّبِيِّينَ وَالصِّدِّيقِينَ وَالشُّهَدَاءِ وَالصَّالِحِينَ ۚ وَحَسُنَ أُولَٰئِكَ رَفِيقًا

"Atakayemtii Allaah na Mtume, basi hao watakuwa pamoja na wale Allaah aliowaneemesha miongoni mwa Manabii, na wakweli, na mashahidi na waja wema - na uzuri ulioje hao kuwa ni rafiki!" (04:69)

Ni lazima pamoja na kumpwekesha Allaah kuwasadikisha Mitume Wake (Swalla Allaahu ´alayhim wa sallam). Kwa ajili hii pindi Allaah alipomtuma Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ilikuwa kazi yake ya kwanza ni kuwalingania watu kumpwekesha Allaah na kuamini kuwa yeye ni Mtume Wake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Kwa hivyo ni lazima kupatikane mambo mawili:

1- Kumpwekesha Allaah na kumtakasia Yeye nia.

2- Ni lazima pia kuwasadikisha Mitume (Swalla Allaahu ´alayhim wa sallam).

Atakayempwekesha Allaah na asiwasadikishe Mitume ni kafiri. Atakayewasadikisha na asimpwekeshe Allaah ni kafiri. Kwa hivyo ni lazima kupatikane mambo yote mawili: kumpwekesha Allaah na kuwasadikisha Mitume (Swalla Allaahu ´alayhim wa sallam).

04. Ulazima wa kuwaamini Mitume wote

Katika nafasi hii tofauti inakuja katika Shari´ah.

Kuhusu kumpwekesha Allaah, kumtakasia Yeye nia, kujiepusha shirki na kuwasadikisha Mitume Wake ni kitu hakuna tofauti kati ya Mitume. Bali hakuna Uislamu, dini, uongofu wala kuokoka isipokuwa kwa kumuabudu Allaah (´Azza wa Jall) peke yake, kumpwekesha katika ´ibaadah, kuamini yale waliyokuja nayo Mitume Wake (Swalla Allaahu ´alayhim wa sallam) kwa njia ya jumla na ya upambanuzi.

Atakayemuabudu Allaah peke yake na asimsadikishe Nuuh katika wakati wake, Ibraahiym katika wakati wake, Huud katika wakati wake, Swaalih katika wakati wake, Ismaa´iyl katika wakati wake, Ishaaq, Ya´quub au wengine waliokuja baada yao akiwemo Mtume wetu Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ni kafiri amemkufuru Allaah (´Azza wa Jall) mpaka awasadikishe Mitume wote na ampwekeshe Allaah (´Azza wa Jall).

05. Maana ya Uislamu

Uislamu katika wakati wa Aadam ilikuwa ni kumpwekesha Allaah pamoja na kufuata Shari´ah ya Aadam (´alayhis-Salaam).

Uislamu katika wakati wa Nuuh ilikuwa ni kumpwekesha Allaah pamoja na kufuata Shari´ah ya Nuuh (´alayhis-Salaam).

Uislamu katika wakati wa Huud ilikuwa ni kumpwekesha Allaah pamoja na kufuata Shari´ah ya Huud (´alayhis-Salaam).

Uislamu katika wakati wa Swaalih ilikuwa ni kumpwekesha Allaah pamoja na kufuata Shari´ah ya Swaalih (´alayhis-Salaam).

Uislamu uliendelea hivo mpaka alipokuja Mtume wetu Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ambapo Uislamu ukawa ni kumpwekesha Allaah pamoja na kuamini yale aliyokuja nayo Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na kufuata Shari´ah yake.

06. Ndio maana mayahudi na manaswara wakakufuru

Mayahudi na manaswara walipokuwa hawakumuamini Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ndipo wakawa makafiri na wapotevu. Hata kama tutakadiria kuwa baadhi yao wanampwekesha Allaah wanazingatiwa kuwa ni wapotevu na makafiri kwa maafikiano ya waislamu. Sababu ni kutomuamini kwao Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam).

Endapo mtu atasema kuwa anamuabudu Allaah peke yake na anamsadikisha Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kwa yote aliyokuja nayo isipokuwa tu katika kuharamisha zinaa ambapo akaonelea kuwa ni halali anazingatiwa kuwa ni kafiri ambaye damu na mali yake ni halali kwa maafikiano ya waislamu. Kadhalika iwapo atasema kuwa anampwekesha na kumuabudu Allaah peke yake pasi na mwengine na anawasadikisha Mitume wote isipokuwa tu katika uharamu wa liwati ambayo maana yake ni mwanaume kumwingilia mwanaume mwenzie. Mtu huyu anahesabika ni kafiri ambaye damu na mali yake ni halali kwa maafikiano ya waislamu. Haya yatakuwa baada ya kubainishiwa dalili ikiwa kweli mtu kama yeye anaweza kuwa hayajui hayo. Tawhiyd na imani yake havitomfaa kitu kwa kuwa amemkadhibisha Mtume na amemkadhibisha Allaah katika baadhi ya mambo. Vivyo hivyo endapo atampwekesha Allaah lakini hata hivyo akacheza shere na Mtume katika kitu, akamtukana katika kitu au baadhi ya Mitume anakuwa kafiri. Amesema (Ta´ala):

قُلْ أَبِاللَّهِ وَآيَاتِهِ وَرَسُولِهِ كُنتُمْ تَسْتَهْزِئُونَ لَا تَعْتَذِرُوا قَدْ كَفَرْتُم بَعْدَ إِيمَانِكُمْ

“Je, mlikuwa mnamfanyia istihizai Allaah na Aayah Zake na Mtume Wake?” Msitoe udhuru. Mmekwishakufuru baada ya kuamini kwenu.” [3] **(09:65-66)**

Ikafahamisha kwamba mwanzoni walikuwa waumini na pindi waliposema maneno haya wakakufuru – Allaah atukinge. Pamoja na kuwa walisema kimzaha tu na kimchezo.

[3] Tazama ”al-Jaamiy´ al-Bayaan fiy Tafsiyr” ya Ibn Jariyr at-Twabariy (01/19-20) na ”Tafsiyr-ul-Qur-aan al-´Adhwiym” ya Ibn Kathiyr (02/351-352).

07. Kinyume cha Tawhiyd ni shirki

Kinyume cha Tawhiyd hii ni kumshirikisha Allaah (´Azza wa Jall). Kila kitu kina kinyume. Kinyume kinabainishwa kwa kinyume. Baadhi ya washairi wamesema:

Kinyume hubaini uzuri wake kinyume chake

Kwa kupatikana kinyume chake mambo yanapata kupambanuka

Kumshirikisha Allaah ndio kinyume cha Tawhiyd ambayo Allaah amewatuma kwayo Mitume Wake (Swalla Allaahu ´alayhim wa sallam). Mshirikina ameitwa kuwa ni mshirika kwa kuwa ameshirikisha pamoja na Allaah wengine katika mambo ambayo ni ´ibaadah inayomuhusu Allaah pekee, katika mambo yanayohusiana na ufalme na kuwaendesha waja Wake na kutomsadikisha katika yale aliyoeleza au kuyaweka katika Shari´ah. Kwa ajili hiyo ndio maana akawa ni mwenye kumshirikisha Allaah na katika ile shirki aliyomtumbukia ndani yake.

08. Maana ya Shahaadah

Kumpwekesha Allaah ndio maana ya ´hapana mungu isipokuwa Allaah`. Bi maana hapana muabudiwa wa haki isipokuwa Allaah. Ni kukanusha ustahiki wa ´ibaadah kwa asiyekuwa Allaah na badala yake kumthibitishia Allaah pekee. Amesema (Subhaanah):

ذَٰلِكَ بِأَنَّ اللَّهَ هُوَ الْحَقُّ وَأَنَّ مَا يَدْعُونَ مِن دُونِهِ الْبَاطِلُ

“Hivyo ni kwa kuwa Allaah ndiye wa kweli na kwamba wale wanaowaomba badala Yake ni batili.” (31:30)

فَاعْلَمْ أَنَّهُ لَا إِلَٰهَ إِلَّا اللَّهُ

“Basi tambua ya kwamba hapana mungu wa haki isipokuwa Allaah.” (47:19)

شَهِدَ اللَّهُ أَنَّهُ لَا إِلَٰهَ إِلَّا هُوَ وَالْمَلَائِكَةُ وَأُولُو الْعِلْمِ قَائِمًا بِالْقِسْطِ ۚ لَا إِلَٰهَ إِلَّا هُوَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ

“Allaah, Malaika Wake na wale wenye elimu wameshuhudia ya kwamba hapana mungu wa haki isipokuwa Yeye – Yeye ndiye Mwenye kusimamisha kwa uadilifu. Hapana mungu isipokuwa Yeye ni Mwenye nguvu kabisa, Mwenye hikmah wa yote.” (03:18)

وَقَالَ اللَّهُ لَا تَتَّخِذُوا إِلَٰهَيْنِ اثْنَيْنِ ۖ إِنَّمَا هُوَ إِلَٰهٌ وَاحِدٌ

“Allaah anasema: “Msijichukulie waungu wawili. Hakika Yeye ndiye mungu wa haki mmoja.”” (16:51)

Kumpwekesha Allaah ni kumuabudu Allaah peke yake kwa imani, ukweli na matendo na sio maneno peke yake pamoja na kuamini kwamba kumuabudu mwengine asiyekuwa Yeye ni batili na kwamba mwenye kumuabudu mwengine asiyekuwa Yeye ni mshirikia. Pamoja vilevile na kujitenga nao mbali. Amesema (´Azza wa Jall):

قَدْ كَانَتْ لَكُمْ أُسْوَةٌ حَسَنَةٌ فِي إِبْرَاهِيمَ وَالَّذِينَ مَعَهُ إِذْ قَالُوا لِقَوْمِهِمْ إِنَّا بُرَآءُ مِنكُمْ وَمِمَّا تَعْبُدُونَ مِن دُونِ اللَّهِ كَفَرْنَا بِكُمْ وَبَدَا بَيْنَنَا وَبَيْنَكُمُ الْعَدَاوَةُ وَالْبَغْضَاءُ أَبَدًا حَتَّىٰ تُؤْمِنُوا بِاللَّهِ وَحْدَهُ

“Hakika mna kigezo bora kwa Ibraahiym na wale walio pamoja naye walipowaambia watu wao: “Hakika sisi tumejitenga nanyi mbali na yale mnayoyaabudu badala ya Allaah; tunakukanusheni na umedhihirika baina yetu na baina yenu uadui na chuki milele mpaka mumuamini Allaah pekee.”” (60:04)

وَإِذْ قَالَ إِبْرَاهِيمُ لِأَبِيهِ وَقَوْمِهِ إِنَّنِي بَرَاءٌ مِّمَّا تَعْبُدُونَ إِلَّا الَّذِي فَطَرَنِي فَإِنَّهُ سَيَهْدِينِ

“Pindi Ibraahiym alipomwambia baba yake na watu wake: “Hakika mimi ni mwenye kujitenga mbali kabisa na yale mnayoyaabudu - isipokuwa ambaye ameniumba, basi hakika Yeye ataniongoa.”” (43:26-27)

Unatakiwa kujitenga mbali na kumuabudu asiyekuwa Allaah na vile wanavyoviabudu.

Makusudio ni kwamba ni lazima kumpwekesha Allaah kwa kumuabudu Yeye peke yake na wakati huo huo kujitenga mbali na kuabudu asiyekuwa Yeye.

09. Kuhukumu kwa Shari´ah ni sehemu katika Tawhiyd

Ni lazima vilevile mtu kuamini ubatilifu wa shirki na kwamba ni wajibu kwa viumbe wote majini na watu wamkhusishe Allaah kwa ´ibaadah na kuitekelezea Tawhiyd hii haki yake kwa kuhukumu na Shari´ah ya Allaah. Hakika Allaah (Subhaanahu wa Ta´ala) ndiye Mwenye kuhukumu.

Katika Tawhiyd kunaingia kuamini na kusadikisha hilo. Yeye ndiye Mwenye kuhukumu duniani kwa Shari´ah Yake na Aakhirah Yeye mwenyewe (Subhaanahu wa Ta´ala). Amesema (´Azza wa Jall):

إِنِ الْحُكْمُ إِلَّا لِلَّهِ

“Hakuna hukumu isipokuwa ya Allaah.” (06:57)

فَالْحُكْمُ لِلَّهِ الْعَلِيِّ الْكَبِيرِ

“Basi leo hukumu ni ya Allaah pekee, Aliye juu, Mkubwa.” (40:12)

وَمَا اخْتَلَفْتُمْ فِيهِ مِن شَيْءٍ فَحُكْمُهُ إِلَى اللَّهِ

”Katika lolote lile mlilokhitilafiana, basi hukumu yake ni kwa Allaah.” (42:10)

10. Baadhi ya sura za shirki na kufuru

Kuwafanyia baadhi ya ´ibaadah mawalii, Mitume, jua, mwezi, jini, Malaika, masanamu, miti na vinginevyo yote haya yanaitengua na kuibatilisha Tawhiyd.

Ukitambua kuwa Allaah (Subhaanah) alimtuma Mtume Wake Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na Mitume wengine waliokuwa kabla yake kuwaendea watu waliokuwa wanawaabudu asiyekuwa Allaah. Miongoni mwao kuna waliokuwa wakiabudu Mitume, waja wema, miti, mawe, masanamu yaliyochongwa, nyota na vinginevyo. Aliwalingania (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) wote katika kumpwekesha Allaah, kumuamini na kutamka shahaadah, wajitenge mbali na yale yanayoenda kinyume nayo na waungu wao na kwamba anayefanya baadhi ya ´ibaadah kumfanyia asiyekuwa Allaah hakumpwekesha Allaah. Amesema (Subhaanah):

وَلَقَدْ بَعَثْنَا فِي كُلِّ أُمَّةٍ رَّسُولًا أَنِ اعْبُدُوا اللَّهَ وَاجْتَنِبُوا الطَّاغُوتَ

"Hakika tulituma katika kila ummah Mtume [awaamrishe watu wake] kwamba: "Mwabuduni Allaah na jiepusheni na twaaghuut [miungu ya uongo]."" (16:36)

Kwa haya unapata kutambua kuwa yale yanayofanywa kwenye makaburi yanayoabudiwa badala ya Allaah kama mfano wa kaburi al-Badawiy, al-Husayn huko Misri na mengineyo na yale wanayotumbukiaemo baadhi ya mahujaji na wengineo wanapoomba uokozi, nusura dhidi ya maadui, kuomba msaada na kuleta mashtaka kwenye kaburi la Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ni kumuabudu asiyekuwa Allaah (´Azza wa Jall) na kwamba hii ni shirki ya kipindi cha kwanza cha kishirikina.

Kadhalika yale wanayotumbukia baadhi ya Suufiyyah wanapoitakidi kuwa baadhi ya mawalii wanaendesha ulimwengu ni shirki kubwa katika uola (*Rubuubiyyah*).

Vivyo hivyo yale wanayoitakidi baadhi ya watu ya kwamba baadhi ya viumbe wana mafungamano na Mola (´Azza wa Jall) na kwamba hilo linawatosheleza wao na kumfuata Mtume Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam),

kwamba anajua mambo yaliyofichikana, anaendesha walimwengu na mfano wa hayo ni kumkufuru Allaah kufuru kubwa na shirki ya wazi inayomtoa mwenye nayo katika Uislamu endapo atakuwa anajinasibisha nao.

11. Maana ya ´ibaadah

Hapana Tawhiyd, Uislamu, imani na uokozi isipokuwa kwa kumpwekesha Allaah katika ´ibaadah na kuamini kuwa Yeye ndiye Mfalme wa wafalme, Mwenye kuyaendesha mambo na kwamba Yeye ni mkamilifu katika dhati, sifa, majina na matendo Yake na kwamba Yeye hana mshirika, anayefanana Naye na kwamba halinganishwi na viumbe Wake (´Azza wa Jall). Yeye ndiye ana ukamilifu usiofungamana katika dhati, sifa na matendo Yake. Yeye ndiye Mwendeshaji na Mfalme (´Azza wa Jall). Hakuna yeyote wa kupinga na hukumu Yake. Huku ndio kumpwekesha Allaah. Huku ndio kumuabudu Allaah peke yake. Hii ndio dini ya Mitume wote na ndio maana ya maneno Yake (Ta´ala):

إِيَّاكَ نَعْبُدُ وَإِيَّاكَ نَسْتَعِينُ

“Wewe pekee ndiye tunakuabudu na Wewe pekee tunakuomba msaada." (01:05)

Bi maana Wewe pekee ndiye tunakupwekesha, tunakutii, tunakutarajia na tunakukhofu. Hivyo ndivyo alivyosema Ibn ´Abbaas (Radhiya Allaahu ´anhumaa). Tunakuabudu, tunakutarajia na tunakukhofu peke yako. Wewe ndiye tunakutaka msaada juu ya utiifu na katika mambo yetu yote.

´Ibaadah ni kumpwekesha Allaah (´Azza wa Jall) na kumtakasia katika kutii maamrisho Yake na kujiepusha na makatazo Yake (Subhaanahu wa Ta´ala) pamoja na kuwa na imani kamilifu ya kwamba Yeye ndiye Mwenye kustahiki ´ibaadah, kwamba Yeye ndiye Mola wa walimwengu, Mwenye kuwaendesha viumbe Wake, Mfalme wa kila kitu, Muumbaji wa kila kitu na kwamba Yeye ni mkamilifu katika dhati, majina na matendo Yake na kwamba hana upungufu, kasoro na wala hana mshirika kwa chochote katika hayo (Subhaaahu wa Ta´ala). Bali ana ukamilifu usiofungamana katika kila kitu.

12. Uwajibu wa kuwasadikisha Mitume wote na ukafiri wa anayedai utume na wafuasi wake

Kuanzia hapa tunapata kujua kuwa ni wajibu kuwasadikisha Mitume wote katika yale waliyokuja nayo na katika kilele chao kunakuja Mtume wetu Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na kwamba vovyote mja atamtakasia ´ibaadah Allaah peke yake na akawasadikisha Mitume (Swalla Allaahu ´alayhim wa sallam) na khaswa Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na akajisalimisha kwa Shari´ah yake. Lakini hata hivyo akateleza kufanya kitenguzi kimoja au vingi vinavyoutengua Uislamu ´ibaadah zake zinatenguka na matendo yake ya Uislamu alionayo hayatomfaa kitu. Iwapo kwa mfano atamsadikisha Muhammad katika kila kitu na akajisalimisha kwa Shari´ah yake katika kila kitu. Lakini pamoja na hivyo akasema kuwa Musaylamah ni Mtume pamoja na Muhammad - Musaylamah mwongo ambaye alijitokeza al-Yamaan na Maswahabah wakampiga vita katika zama za as-Swiddiyq (Radhiya Allaahu ´anh) – haya yanabatilisha ´Aqiydah yake, matendo yake na kufunga kwake mchana, kusimama kwake usiku na matendo yake mengine hayatomfaa kitu kwa kuwa amefanya moja ya kitenguzi cha Uislamu ambapo amemsadikisha Musalymah mwongo. Vilevile hilo linapelekea kumkadhibisha Allaah (Subhaanah) pale aliposema:

مَّا كَانَ مُحَمَّدٌ أَبَا أَحَدٍ مِّن رِّجَالِكُمْ وَلَٰكِن رَّسُولَ اللَّهِ وَخَاتَمَ النَّبِيِّينَ

“Hakuwa Muhammad baba wa yeyote miongoni mwa wanaume wenu, lakini ni Mtume wa Allaah na ni mwisho wa Manabii.” (33:40)

Vilevile linapelekea kumkadhibisha Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) katika maneno yake yaliyopokelewa kwa mapokezi mengi ambapo (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema kuwa yeye ndiye Mtume wa nwisho.

13. Kitenguzi kimoja cha Uislamu kinabatilisha matendo yote

Kadhalika atakayefunga mchana na akasimama usiku kutwa, akamuabudu na kumpwekesha Allaah kwa ´ibaadah na akamfuata Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Halafu baada ya yote haya ikatokea, katika wakati wowote ule, akatekeleza baadhi ya ´ibaadah kumfanyia asiyekuwa Allaah kama mfano wa Mtume, walii fulani, sanamu fulani, jua, mwezi na nyota fulani akawa anaiomba, anataka nusura na msaada, kutoka kwake matendo yake yote yaliyotangulia yanabatilika. Hali itaendelea kuwa hivo mpaka pale ataporejea kutubu kwa Allaah (´Azza wa Jall). Amesema (Ta´ala):

وَلَوْ أَشْرَكُوا لَحَبِطَ عَنْهُم مَّا كَانُوا يَعْمَلُونَ

"Lau wangemshirikisha bila shaka yangebatilika yale waliyokuwa wakitenda." (06:88)

وَلَقَدْ أُوحِيَ إِلَيْكَ وَإِلَى الَّذِينَ مِن قَبْلِكَ لَئِنْ أَشْرَكْتَ لَيَحْبَطَنَّ عَمَلُكَ وَلَتَكُونَنَّ مِنَ الْخَاسِرِينَ

"Hakika umefunuliwa Wahy wewe na kwa wale waliokuwa kabla yako ya kwamba ukifanya shirki bila shaka zitabatilika ‘amali zako na [Aakhirah] utakuwa miongoni mwa waliokhasirika." (39:65)

Hali kadhalika iwapo atamuamini na kumsadikisha Allaah katika kila kitu isipokuwa tu katika zinaa ambapo akasema kuwa uzinzi unaruhusu, liwati inaruhusu au pombe inaruhusu kwa haya anakuwa kafiri.

Endapo atafanya kila kitu kilichowekwa katika dini na akahalalisha yale aliyoharamisha Allaah katika yale mambo ambayo yanajulikana fika katika Uislamu anakuwa kafiri kwa kuhalalisha kwake huku na mwenye kuritadi kutoka katika Uislamu. Matendo yake na kumpwekesha kwake Allaah hakutomfaa kitu kwa mujibu wa waislamu wote.

Vilevile ikiwa atasema kuwa Nuuh, Huud, Swaalih, Ibraahiym, Ismaa´iyl au mwengine sio Mtume anakuwa amemkufuru Allaah na matendo yake yote ni batili kwa sababu amemkadhibisha Allaah katika yale aliyokhabarisha kuhusu wao.

Vivyo hivyo akiharamisha vile alivyohalalisha Allaah na wakati huo huo akampwekesha Allaah, akamtakasia ´ibaadah na kuwaamini Mitume kwa mfano akasema kuwa yeye hahalalishi ngamia, ngo´ombe, kondoo au vinginevyo ambavyo amehalalisha Allaah katika vile ambayo kuna maafikiano juu ya uhalali wake na yeye akawa anaonelea kuwa sio halali kwa hayo anakuwa mwenye kukufuru na mwenye kuritadi kutoka katika Uislamu. Hayo yatapitika baada ya kubainishiwa dalili ikiwa mtu mfano wake anaweza kweli kuwa hayajui hayo.

Hayo yanayohusu kinyume chake yule mwenye kuhalalisha alivyoharamisha Allaah. Kwa mfano akawepo mtu mwenye kusema kuwa yeye hahalalishi ngano wala shayiri na kwamba ni haramu anakuwa kafiri. Au akasema kuwa yeye anamhalalisha binti au dada yake anakuwa amemkufuru Allaah na mwenye kuritadi kutoka katika Uislamu hata kama ataswali, atafunga na akafanya ´ibaadah zingine. Kwa sababu moja katika sifa hizi zinabatilisha dini Yake. Amesema (Ta´ala):

وَلَوْ أَشْرَكُوا لَحَبِطَ عَنْهُم مَّا كَانُوا يَعْمَلُونَ

"Lau wangemshirikisha bila shaka yangebatilika yale waliyokuwa wakitenda." (06:88)

14. Watu walivyoipuuza elimu ya dini hii leo

Sisi hii leo katika wakati wetu huu ujinga umekuwa mwingi na elimu imekuwa chache na watu – isipokuwa wale aliotaka Allaah - wamekimbilia katika elimu na mambo mengine yanayohusiana na dunia ambapo matokeo yake elimu yao juu ya Allaah na dini yao imekuwa chache kwa kuwa wameshughulishwa na vile vyenye kuwazuia nayo. Masomo mengi yamekuwa ni yenye kuhusiana na dunia. Kuhusu kujifunza dini ya Allaah, kuizingatia Shari´ah yake na kumpwekesha ni mambo wengi wameyapuuza na wamekuwa wale wenye kujishughulisha nayo hii leo ni wachache mno.

Mja wa Allaah! Unatakiwa kuzingatia jambo hili na ukimbilie katika Qur-aan an Sunnah na kuvidurusu, kuvizingatia na kuvielewa ili uweze kuielewa Tawhiyd ya Allaah, kumuamini na ili vilevile uweze kuelewa ni nini maana ya kumshirikisha Allaah, uwe na uelewa juu ya dini Yake na ili pia uweze kutambua sababu zinazopelekea kuingia Peponi na kuokoka kutokamana na Moto. Haya yote pamoja vilevile na kuhudhuria mizunguko ya kielimu pamoja na kusoma na wanachuoni ili uweze kufaidika wewe na uwafaidishe wengine na uwe juu ya ubainifu na juu ya uelewa katika jambo lako.

15. Hukumu ya mwenye kufa katika shirki kubwa na madhambi

Shirki imegawanyika aina mbili:

Ya kwanza: Shirki kubwa.

Ya pili: Shirki ndogo.

Shirki aina kubwa inapingana na kumpwekesha Allaah, Uislamu na vilevile inaharibu matendo yote. Mshirikina aina hii yuko Motoni. Dalili zimethibitisha kuwa matendo na maneno yake yote amemkufuru Allaah. Kwa mfano kuwaomba uokozi maiti, masanamu, kuonelea halali vile alivyoharamisha Allaah, kuonelea haramu vile alivyohalalisha Allaah au kuwakadhibisha baadhi ya Mitume Wake. Mambo haya yanaharibu matendo na yanapelekea kumritadisha kutoka katika Uislamu. Tumetangulia kubainisha hayo. Amesema (Ta´ala) katika Suurah "an-Nisaa´":

إِنَّ اللَّهَ لَا يَغْفِرُ أَن يُشْرَكَ بِهِ وَيَغْفِرُ مَا دُونَ ذَٰلِكَ لِمَن يَشَاءُ ۚ وَمَن يُشْرِكْ بِاللَّهِ فَقَدِ افْتَرَىٰ إِثْمًا عَظِيمًا

"Hakika Allaah hasamehi kushirikishwa na anasamehe yaliyo chini ya hayo kwa amtakae. Yeyote atakayemshirikisha Allaah, basi hakika amebuni dhambi kuu." (04:48)

Hapa Allaah ameweka wazi kuwa hasamehi shirki na akafungamanisha yaliyo chini ya hiyo shirki na matakwa Yake (Subhaanahu wa Ta´ala). Ina maana kwamba akitaka atayasamehe na akitaka atamuadhibu kiasi cha madhambi yake aliokufa juu yake pasi na kutubia. Baada ya kumsafisha na Moto atamtoa humo na kumweka Peponi. Haya ni kwa maafikiano ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah tofauti na wanavyoonelea Khawaarij, Mu´tazilah na waliofuata mfumo wao. Kuhusu yaliyokuja katika Suurah "az-Zumar" amejumuisha na kutofungamanisha. Amesema (Subhaanah):

قُلْ يَا عِبَادِيَ الَّذِينَ أَسْرَفُوا عَلَىٰ أَنفُسِهِمْ لَا تَقْنَطُوا مِن رَّحْمَةِ اللَّهِ ۚ إِنَّ اللَّهَ يَغْفِرُ الذُّنُوبَ جَمِيعًا ۚ إِنَّهُ هُوَ الْغَفُورُ الرَّحِيمُ

“Sema: “Enyi waja Wangu ambao wamepindukia mipaka juu ya nafsi zao: ´Msikate tamaa na rehema za Allaah. Hakika Allaah anasamehe dhambi zote. Hakika Yeye ni Mwingi wa kusamehe, Mwenye kurehemu.´” (39:53)

Wanachuoni wamesema kuwa Aayah hii inawahusu wale waliotubia. Kuhusu Aayah ya Suurah “an-Nisaa´” haiwahusu wale waliotubia isipokuwa ni wale waliokufa juu ya shirki hali ya kuwa ni mwenye kuendelea na baadhi ya maasi. Hiyo ndio maana ya maneno Yake (Subhaanah):

إِنَّ اللَّهَ لَا يَغْفِرُ أَن يُشْرَكَ بِهِ وَيَغْفِرُ مَا دُونَ ذَٰلِكَ لِمَن يَشَاءُ

"Hakika Allaah hasamehi kushirikishwa na anasamehe yaliyo chini ya hayo kwa amtakae.” (04:48)

Khawaarij wanaonelea kuwa watenda madhambi watadumishwa Motoni milele na kwa maasi yake hayo ni kafiri. Mu´tazilah wameafikiana nao kuonelea kuwa atadumishwa Motoni milele. Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah wamewakhalifu katika hilo na wanaonelea kuwa mzinifu, mwizi na mwenye kuwaasi wazazi wake na watenda madhambi makubwa wengineo hawakufuru kwa hilo na hawatodumishwa Motoni milele maadamu hawajahalalisha madhambi hayo. Bali wako chini ya matakwa ya Allaah kama tulivyotangulia kusema. Haya ni mambo makubwa ambayo tunapaswa kuyatambua na tuyafahamu vizuri kwa kuwa ni katika misingi ya ´Aqiydah.

16. Muislamu kutenga wakati kwa ajili ya kujifunza dini yake

Muislamu anatakiwa kufahamu uhakika wa dini yake na kinyume chake ambacho ni shirki na atambue vilevile kuwa mlango wa kutubu juu ya shirki na madhambi uko wazi mpaka pale Qiyaamah kitaposimama.

Msima mkubwa ni mtu kughafilika na dini ya Allaah na kutojifunza nayo. Huenda akatumbukia katika shirki na kufuru bila yeye kujali kwa sababu ya ujinga na kutokuwa na elimu juu ya yale aliyokuja nayo Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) katika uongofu na dini ya haki.

Ee mwerevu! Izindue nafsi yako, yaadhimishe maharamisho ya Mola Wako, mtakasie matendo Allaah, kimbilia katika kheri na uitambue dini yako kwa dalili zake, jifunze Qur-aan na Sunnah. Fanya hivo kwa kukimbilia katika Kitabu cha Allaah, kwa kuhudhuria mizunguko ya kielimu na kwa kusuhubiana na matangamano mazuri mapaka uweze kuijua dini yako. Kithirisha kumuomba Mola Wako uthabiti juu ya uongofu na haki. Utapotumbukia katika maasi kimbilia kufanya tawbah:

“Kila binaadamu ni mwenye kukosea sana. Mbora katika wakoseaji ni yule mwenye kutubia.”[4]

Hivyo ndivyo ilivyokuja katika Hadiyth Swahiyh. Maasi ni upungufu katika dini na ni udhaifu katika imani.

Kwa hivyo ala ala kimbilia katika tawbah, ujikwamue nayo na ujutie. Allaah anamsamehe yule mwenye kutubia. Yeye ndiye amesema (Subhaanah):

وَتُوبُوا إِلَى اللَّهِ جَمِيعًا أَيُّهَ الْمُؤْمِنُونَ لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ

“Tubuni kwa Allaah nyote, enyi waumini, ili mpate kufaulu.” (24:31)

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا تُوبُوا إِلَى اللَّهِ تَوْبَةً نَّصُوحًا

”Enyi mlioamini! Tubieni kwa Allaah tawbah ya kwelikweli.” (66:08)

[4] at-Tirmidhiy (2499), Ibn Maajah (4251), Ahmad (03/198) na ad-Daarimiy (2727).

Ni lazima kutubia. Tawbah ni jambo lenye kulazimiana na mja daima. Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

“Tawbah inafuta yaliyokuwa kabla yake.”

Nyooka kwa hilo. Kila unapoteleza kimbilia kutubia na kutengeneza. Kuwa ni mwenye kujifunza dini. Fungu lako la dunia lisikushughulishe na fungu lako la Aakhirah. Tenge wakati kwa ajili ya dunia yako, utenge vilevile wakati kwa ajili ya kujifunza dini yako, kusoma, kujikumbusha, kuitilia umuhimu Qur-aan na Sunnah, kuhudhuria mizunguko ya kielimu, kutangamana na ufanye wakati wako mwingi unatangamana na watu wema. Hili ndio muhimu zaidi kwako na ndio sababu ya kuokoka kwako.

17. Shirki ndogo na aina zake

Aina ya pili ni shirki ndogo. Mfano wake ni kama kujionyesha, kutaka kusikika katika baadhi ya matendo na maneno, kusema "Allaah akitaka na fulani" na kuapa kwa asiyekuwa Allaah kama mtu akaapa kwa amana, Ka´bah, Mtume na mfano wa hayo. Haya na mfano wake yanaingia katika shirki ndogo. Ni wajibu kutahadhari na hayo. Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alisema wakati mtu alipomwambia: "Allaah akitaka na wewe" ambapo akasema: "Umenifanya kuwa mshirika wa Allaah? Sema: "Akitaka Allaah peke yake."[5]

Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

"Msiseme "Allaah akitaka na fulani". Badala yake semeni: "Allaah akitaka kisha fulani.""[6]

"Anayetaka kuapa basi na aape kwa Allaah au anyamaze."[7]

"Msiape kwa baba zenu, mama zenu, washirika wenu na wala msiape kwa Allaah isipokuwa muwe wakweli.[8]

"Anayeapa kwa asiyekuwa Allaah amefanya shirki."[9]

Kuna Hadiyth zingine Swahiyh zilizothibiti zikiwa na maana kama hii. Miongoni mwazo ni yale yaliyosema (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

"Kikubwa ninachokikhofia kwenu ni shirki ndogo. Alipoulizwa akasema kuwa ni kujionyesha."[10]

---

[5] at-Tirmidhiy (2806), an-Nasaa´iy (5365), Abu Daawuud (4158), Ibn Maajah (2117) na Ahmad (01/347).

[6] Abu Daawuud (4980) na Ahmad (05/399).

[7] al-Bukhaariy (2679), Muslim (1646), at-Tirmidhiy (1534), Abu Daawuud (3249) na wengineo.

[8] an-Nasaa´iy (3769), Abu Daawuud (3248).

[9] al-Bukhaariy (6108), Muslim (1646), at-Tirmidhiy (1535), an-Nasaa´iy (3766), Abu Daawuud (3251), Ibn Maajah (2094), Ahmad (02/69) na wengineo.

[10] Ahmad (05/428).

Kujionyesha wakati mwingine kunaweza kuwa kufuru kubwa pale ambapo mtu ataingia katika Uislamu kwa kujionyesha na kwa unafiki na akadhihirisha Uislamu na sio kwa ajili ya kuuamini wala kwa ajili ya kuupenda. Kwa haya mtu huyo anakuwa mnafiki na kafiri aliyekufuru kufuru kubwa.

Kadhalika mtu akiapa kwa asiyekuwa Allaah, akamuadhimisha yule aliyeapa kwa jina lake kama anavyomuadhimisha Allaah, akaamini kuwa anajua mambo yaliyofichikana au akaonelea kuwa ni sawa akaabudiwa pamoja na Allaah (Subhanaah), kwa haya anakuwa kafiri na mshirikina aliyeshirikisha shirki kubwa. Ama ikiwa ni jambo limempitikia tu mdomoni na akawa ameapa kwa asiyekuwa Allaah kama vile kwa Ka´bah, Mtume na vinginevyo – pasi na kuwa na imani hii – anakuwa mshirikina aliyeshirikisha shirki ndogo tu.

Ninamuomba Allaah (´Azza wa Jall) atutunuku sote uelewa wa kuweza kuielewa dini yake, uimara juu yake, aturuzuku sote kuwa na msimamo juu yake, atukinge sote kutokamana na shari ya nafsi zetu na uovu wa matendo yetu na fitina zenye kupotosha – hakika Yeye (Ta´ala) ni Mwingi wa kutoa na ni mkarimu.

Swalah na salaam na baraka zimwendee mja na Mtume Wake, Mtume wetu Muhammad, kizazi chake, Maswahabah wake na watakaowafuata kwa wema hadi siku hiyo ya mwisho.